TANGAZO LA SERIKALI Na. 107 la tarehe 16/2/2024

SHERIA YA MIPANGOMIJI,
(SURA YA 355)

______

# AMRI

______

*(Imetengenezwa chini ya kifungu cha 8(1) na 23(1))*

AMRI YA KURASIMISHA MAKAZI YASIYOPANGWA KATIKA ENEO LA ILEMBO YA MWAKA 2024

Jina

1. Amri hii itajulikana kama Amri ya Kurasimisha Makazi Yasiyopangwa Katika Eneo la Ilembo ya mwaka 2024.

Utangazaji wa Eneo la Upangaji Sura ya 355

2. Eneo lililoainishwa katika Jedwali la Amri hii linatangazwa kuwa eneo la upangaji kwa madhumuni ya Sheria ya Mipangomiji.

Mpangokina wa eneo

3. Mpangokina wa eneo lililoainishwa katika Jedwali unaandaliwa na kuhifadhiwa kwa Mkurugenzi wa Mipangomiji na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya.

JEDWALI

*(Limeandaliwa chini ya aya ya 2)*

Eneo la upangaji lipo ndani ya mipaka ifuatavyo:

“Mpaka unaanzia kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H10 yenye majira-nukta 539560MS, 8983286KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.6 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H11 yenye majira-nukta 539250MS, 8982779KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H12 yenye majira-nukta 539308MS, 8982637KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H13 yenye majira-nukta 539308MS, 8982547KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H14 yenye majira-nukta 539047MS, 8982506KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H15 yenye majira-nukta 539219MS, 8982361KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Magharibi kwa umbali wa kilomita 0.7 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H16 yenye majira-nukta 538593MS, 8981950KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini kwa kufuata mto Tawajito kwa umbali wa kilomita 2.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H1 yenye majira-nukta 537935MS, 898388KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H2 yenye majira-nukta 538190MS, 898366KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H3 yenye majira-nukta 538165MS, 8983590KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini - Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H4 yenye majira-nukta 538367MS, 8983655KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini- Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.3 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H5 yenye majira-nukta 538529MS, 8983501KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kaskazini- Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H6 yenye majira-nukta 538844MS, 8983485KZ;baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini- Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H7 yenye majira-nukta 538940MS, 8983485KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini-Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.4 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H8 yenye majira-nukta 539253MS, 8983279KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Kusini- Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.1 hadi kwenye alama ya mpaka ya upimaji namba H9 yenye majira-nukta 539373MS, 8983244KZ; baada ya hapo mpaka unaelekea Mashariki kwa umbali wa kilomita 0.2 hadi ulipoanzia.”

Dodoma,
29 Disemba, 2023

JERRY WILLIAM SILAA,
*Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi*